**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SHERIA YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

## SURA YA 391, TOLEO LA 2021

IMEPIGWA CHAPA NA MPIGA CHAPA WA SERIKALI, DAR ES SALAAM-TANZANIA

# SHERIA YA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

## SURA YA 391

----------------------

## MPANGILIO WA VIFUNGU

----------------------------

**FUNGU** **Jina**


### SEHEMU YA I

### MASHARTI YA UTANGULIZI

1. **Jina Fupi na kuanza kutumika**
2. **Katiba**
3. **Kutumika**
4. **Tafsiri**

### SEHEMU YA II

### TUME

5. **Sheria ya kusimamia Tume.**
6. **Majukumu ya Tume.**
7. **Muundo.**
8. **Muda na masharti ya ajira.**
9. **Wajumbe kuacha baadhi ya nafasi zao.**
10. **Kuondolewa kazini kwa Makamishna.**
11. **Katibu Mtendaji na watumishi wengine wa Tume.**
12. **Viapo.**

### SEHEMU YA III
### HADHI, MAMLAKA NA UWEZO WA TUME

13. **Tume idara ya umma.**
14. **Uhuru wa Tume.**
15. **Mamlaka ya Tume.**
16. **Ukomo na Mipaka ya uchunguzi.**
17. **Hadhi ya mienendo, maamuzi na mashahidi.**
18. **Usikilizaji mashauri hadharani**
19. **Uficho na usiri.**
20. **Utaratibu wa kusikiliza shauri**
21. **Vikao na maamuzi ya Tume.**

**SEHEMU YA IV**
**MALALAMIKO NA UCHUNGUZI**

**22. Namna ya kuwasilisha malalamiko.**
**23. Uwakilishi.**
**24. Taarifa ya lalamiko na fursa ya kusikilizwa.**
**25. Mamlaka maalum ya uchunguzi.**
**26. Utaratibu wa kufanya uchunguzi.**
**27. Ushahidi wakati wa uchunguzi.**
**28. Utaratibu baada ya uchunguzi.**

**SEHEMU YA V**
**FEDHA, UKAGUZI NA TAARIFA**

**29. Rasilimali za Tume.**
**30. Uwajibikaji.**
**31. Makadirio ya mapato na matumizi.**
**32. Ukaguzi wa hesabu.**
**33. Taarifa ya mwaka.**
**34. Taarifa maalum.**
**35. Taarifa nyingine**

**SEHEMU YA VI**
**MASHARTI ANUAI/MENGINEYO**

**36. Utaratibu, n.k. wa Tume.**
**37. Makosa na adhabu.**
**38. Kanuni**
**39. Kufutwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 1966**
**40. Muda wa mpito**

**JEDWALI**

**Viapo/Matamko ya Wajumbe na Watumishi wa Tume**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## SURA YA 391

NAKUBALI,
BENJAMIN W. MKAPA,
*Rais*
2 Mei, 2001

**Sheria ya kuweka masharti ya kutekeleza Ibara ya 131 ya Katiba kuhusiana na majukumu, mamlaka, kinga na mambo mengine kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na mambo yanayohusiana na hayo.**

[……………………………………..]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## SEHEMU YA I

### VIFUNGU VYA AWALI

Jina kifupi na kuanza kutumika

**1.** Sheria hii inaweza kutajwa kama Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, 2001 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri anaweza, kwa tangazo lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

Katiba

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Katiba.

Kutumika

**3.** Sheria hii inatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tafsiri

**4.** Katika Sheria hii, isipokuwa muktadha utakavyohitaji vinginevyo-

"Afisa wa Umma" au "Ofisi ya Umma" inamaanisha kila afisa au idara iliyopewa au inayotekeleza majukumu ya umma, na inahusisha afisa au idara iliyo chini ya udhibiti wa mamlaka ya serikali ya mtaa, Jamii au shirika la umma au mamlaka nyingine kwa namna yoyote itakavyoitwa;

"Kamati ya Uteuzi" inamaanisha Kamati iliyoanzishwa na Ibara ya 129(4) ya Katiba;

"Kamishna" na "Kamishna Msaidizi" inamaanisha Mwenyekiti au wajumbe wengine wa Tume walioteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya Katiba;

"Katiba" inamaanisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Mahakama Kuu" inamaanisha Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano au Mahakama Kuu ya Zanzibar;

"Mamlaka husika" inajumuisha mtu yeyote au mamlaka, iwe ya kitaasisi au vinginevyo, ambayo kwake pendekezo limetolewa na Tume chini ya Kifungu cha 28 cha Sheria hii;

"Mjumbe" inamaanisha Kamishna au Kamishna Msaidizi;

"Mwenyekiti" inamaanisha Mwenyekiti wa Tume au, pale itapokuwa, Kamishna anayetekeleza majukumu ya Mwenyekiti;

"Serikali" inahusisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, au mamlaka ya serikali ya mtaa ambayo inatekeleza madaraka au mamlaka yake au kwa niaba ya mamlaka ya serikali ya mtaa;

"Tume" inamaanisha Tume iliyoanzishwa na Ibara ya 129 ya Katiba;

"Uchunguzi" inamaanisha uchunguzi uliofanywa na Tume kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hii;

"Waziri" inamaanisha Waziri, ambaye kwa wakati huo anahusika na masuala ya haki za binadamu;

## SEHEMU YA II

## TUME

Sheria ya kusimamia Tume

**5.** Muundo, majukumu, mamlaka, kinga na masuala yanayohusiana na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliyoanzishwa na Ibara ya 129 ya Katiba yataendeshwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Majukumu ya Tume

**6.**-(1) Tume itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuhamasisha nchini hifadhi na ulinzi wa haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi;

(b) kupokea tuhuma na malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu kwa jumla;

(c) kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;

(d) kufanya utafiti kuhusu haki za binadamu, haki za kiutawala na masuala ya utawala bora na kuelimisha umma kuhusu maswala hayo;

(e) Inapobidi, kufungua mashauri mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kutoa nafuu ya haki iliyovunjwa au zilizovunjwa au ukiukwaji wa misingi ya haki za utawala;

(f) kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika na masharti ya kifungu hiki katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;

(g) kuchunguza au kuhoji malalamiko kuhusiana na mazoea au vitendo vya watu wanaoshikilia ofisi katika utumishi wa serikali, mamlaka ya umma au vyombo vingine ya umma, pamoja na taasisi za kibinafsi na watu binafsi ambapo malalamiko hayo yanadai matumizi mabaya ya madaraka, uonevu, kutotendewa haki kwa mtu yeyote, iwe mlalamikaji au la, wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kiofisi;

(h) kutembelea magereza na sehemu wanamoshikiliwa watu, au sehemu zinazofanana na hizo kwa ajilia ya kufanya tathmni na kukagua hali ya watu wanaoshikiliwa katika sehemu hizo na kutoa mapendekezo ya kurekebisha matatizo yaliyopo kwa mujibu wa sheria hii;

(i) kuchukua hatua za kutoa nafuu, marekebisho, ubadilishaji au ukomeshaji wa matukio yaliyotajwa katika aya za (e), (f), (g) au (h) kupitia njia za haki, sahihi na bora, ikihusisha kufungua mashauri mahakamani;

(j) kutoa ushauri kwa Serikali na vyomno vingine vya umma na vya taasisi za sekta binafsi kuhusu masuala mahsusi yahusuyo haki za binadamu na haki za kiutawala;

(k) kutoa mapendekezo yanayohusu sheria yoyote iliyopo au iliyopendekezwa, kanuni, au masharti ya kiutawala ili kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni na viwango vya haki za binadamu na misingi ya utawala bora;

(l) kuhimiza uridhiaji wa au kuikubali mikataba au makubaliano juu ya haki za binadamu, kuoanisha sheria za nchi na kufuatilia na kutathmini uzingatiaji, ndani ya Jamhuri ya Muungano, na serikali na watu wengine, na viwango vya haki za binadamu vilivyotolewa katika mikataba au makubaliano au chini ya desturi za sheria za kimataifa ambazo Jamhuri ya Muungano inawajibika nazo;

(m) kwa msaada wa Serikali, kushirikiana na taasisi za Umoja wa Mataifa, OAU, Jumuiya ya Madola na taasisi nyingine za pande-mbili, zaidi ya pande-mbili au kikanda na taasisi za kitaifa za nchi nyingine ambazo zina weledi katika maeneo ya ulinzi na uhamasishaji wa haki za binadamu na

haki za kiutawala;

(n) kuchukua hatua zipasazo kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi na suluhu miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume;

(o) kutekeleza majukumu mengine kama yanavyoweza kuwa yametamkwa katika sheria nyingine.

(2)Bila kuathiri masharti ya Kifungu kidogo cha (1), Tume inapaswa, kwa kushirikiana na umma, itatumia uhusiano wake kuhimiza, kulinda na pale inapobidi kutoa msaada kwa mtu ambaye haki zake zimevunjwa au ziko katika hatari ya kuelekea kuvunjwa.

Muundo

**7**.–(1) Tume itaundwa na-

(a) Mwenyekiti, ambaye atakuwa ni mtu mwenye sifa ya kuweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au Jaji wa Mahakama ya Rufaa;

(b) Makamu Mwenyekiti ambaye atateuliwa kwa kuzingatia kanuni kwamba endapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atakuwa ni mtu anayetoka upande mwingine wa Muungano;

(c) Makamishna wengine wasiozidi watano watakaoteuliwa kutoka miongoni mwa watu wenye ujuzi, uzoefu na weledi mkubwa katika mambo yanayohusiana na haki za binadamu, sheria, serikali, siasa au masuala ya kijamii;

(d) Makamishna Wasaidizi.

(2) Rais baada ya kushauriana na Kamati ya Uteuzi, atawateua Makamishna na Makamishna Wasaidizi.

(3) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Kamishna au Kamishna Msaidizi kama anasifa njema za kiwango cha juu na anajulikana kwa maadili ya kiwango cha juu, uadilifu, asiyependelea na mjuvi katika mambo ya haki za binadamu na utawala bora.

(4) Waziri atatunga Kanuni zinazohusu utaratibu utakaofuatwa na Kamati ya Uteuzi na ushirikishaji wa asasi za kiraia katika kutafuta watahiniwa kwa ajili ya kuteuliwa kuwa Makamishna na Makamishna wasaidizi.

Muda na masharti ya ajira
Sheria Na. 16 ya 2001 kif. 3

**8**.-(1) Kamishna atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu na atastahiki kuteuliwa tena kwa muhula mwingine wa pili usiozidi miaka mitatu.

(2) Makamishna watalipwa mishahara, au marupurupu mengine, kama itakavyopangwa na Rais, na mishahara hiyo itatokana na Mfuko Mkuu wa Hazina.

(3) Kamishna anaweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Rais mwezi mmoja kabla.

(4) Nafasi ya Kamishna itakuwa wazi-

(a) kwa Kamishna kujiuzulu au kondolewa kwenye nafasi yake;
(b) kama Kamishna atatangazwa kufilisika;
(c) kwa Kamishna kustaafu au kufariki.

Wajumbe kuacha baadhi ya nafasi zao

**9**.-(1) Pamoja na wadhifa wowote anaoshikilia katika chama chochote cha siasa kwa mujibu wa Ibara ya 129(6) ya Katiba, mtu aliyeteuliwa kuwa Kamishna atatakiwa kuachia, baada tu ya kuteuliwa kuwa Kamishna mtu anayeshikilia wazifa wowote kati ya hizi zifuatazo atatakiwa kuachia ofisi hiyo mara moja, yaani-

(a) Ubunge;
(b) Ujumbe katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
(c) Spika wa Bunge;
(d) Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;
(e) Jaji au wadhifa mwingine wa kimahakama;
(f) Utumishi Serikalini;
(g) Ujumbe wa Tume ya Uchaguzi;
(h) Ujumbe katika mamlaka ya Serikali za Mitaa na utumishi wowote katika mamlaka ya serikali za mtaa;
(i) Nafasi yoyote nyingine katika utumishi wa umma.

(2) Pale ambapo mtu ameteuliwa kuwa Kamishna na kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) ameachia wadhifa wa aina yoyote ulioainishwa chini ya kifungu hicho, isipokuwa wadhifa ambao atatakiwa kwa mujibu wa sheria kuchaguliwa na watu, mtu huyo, iwapo atakoma kuwa Kamishna, anaweza kuteuliwa tena kushika wadhifa huo na mamlaka husika ya uteuzi, na bila kujali masharti ya sheria nyingine au mkataba wa ajira utakaomuathiri mtu huyo vinginevyo, iwapo mtu huyo atateuliwa tena, utumishi wake katika wadhifa kabla ya kuteuliwa kwake utahesabika kuwa unaendelea kwenye wadhifa aliokuwa nao kabla ya uteuzi wake kuwa Kamishna.

(3) Pale ambapo mtu atateuliwa tena kushika wadhifa wowote kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) na utumishi wake kwenye wadhifa ule ukaendelea

kuhesabika kabla ya uteuzi atahesabika kuwa anaendelea na utumishi wake kabla ya kuuacha chini ya kifungu kidogo cha (1)-

(a) kipindi kati ya kuacha wadhifa wake na uteuzi wake mpya kwenye wadhifa wake ule ule hakitahesabika wakati wa kukokotoa kiwango cha pensheni, kiinua mgongo au mafao mengine anayostahili kulipwa pindi atakapostaafu katika wadhifa ule;

(b) kipindi ambacho alifanya kazi kama Kamishna kitahesabika kwa ajili ya kukokotoa hesabu ya muda wa utumishi wake kwenye wadhifa huo ili kujua iwapo mtu huyo anastahili kulipwa pensheni yoyote, kiinua mgongo au mafao mengine ya kustaafu kana kwamba mtu huyo hakuwahi kuacha wadhifa katika kipindi hicho.

(4) Katika kifungu hiki-

"mamlaka husika ya uteuzi" kwa kuhusiana na wadhifa wowote maana yake ni mtu au mamlaka yenye uwezo wa kufanya teuzi kwa wadhifa huo;

Sura ya 298 na 237

"ofisi ya utumishi wa umma" na "afisa wa mahakama" ina maana kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Utumishi wa Mahakama mtawalia.

Kuondolewa kazini kwa Makamishna

**10**.-(1) Kwa kuzingatia Sheria hii, Kamishna anaweza kuondolewa tu kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake, kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine yoyote, au utovu wa nidhamnu kinyume cha maadili ya kazi au sheria yoyote inayohusu maadili ya viongozi wa umma.

(2) Endapo itatokea hoja ya kumuondoa Kamishna na Rais akaridhika kuwa suala hilo lichunguzwe –

(a) atateua tume maalum itakayoundwa na mwenyekiti na wajumbe wengine wasiopungua wawili, Mwenyekiti na angalau nusu ya wajumbe wengine watakuwa ni watu ambao ni Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani ya Tanzania;

(b) tume maalum itafanya uchunguzi na ndani ya siku 90 tangu kuundwa kwake, itatoa taarifa kwa Rais juu ya jambo lote na kushauri iwapo Kamishna husika aondolewe kutoka wadhifa wake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki;

(c) iwapo tume maalum itamshauri Rais kuwa Kamishna husika aondolewe kutoka wadhifa wake kwa mojawapo ya sababu zilizoelezwa katika kifungu kidogo cha (1), basi Rais atamuondoa Kamishna huyo kwenye wadhifa wake.

(3) Endapo hoja ya kuondolewa Kamishna kwenye wadhifa wake imewasilishwa kwa tume maalum kwa kuzingatia kifungu hiki, Rais anaweza kumsimamisha Kamishna husika kutekeleza majukumu yake, na

wakati wowote anaweza kusitisha kumsimamisha na kwa vyovyote kusimamishwa huko kutakoma iwapo tume maalum itamshauri Rais kutokumuondoa kwenye wadhifa Kamishna muhusika.

Katibu Mtendaji na watumishi wengine wa Tume

**11**.-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Tume mbaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Tume kutoka miongoni mwa watu wanaoshikilia au waliowahi kushika nyadhifa za juu katika utumishi wa Serikali.

(2) Mtu hawezi kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji wa Tume isipokuwa kama ana shahada ya sheria kutoka chuo kikuu ambacho tuzo zake za sheria zinatambuliwa na Serikali na aliye na uzoefu katika utawala au menejimenti tangu alipohitimu, awe amefanya kazi za sheria au awe amejishughulisha katika ufundishaji au utafiti katika sheria, kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa ndiye mtendaji mkuu wa Tume na, kwa kuzingatia maelekezo na udhibiti wa jumla wa Tume, atalazimika-

(a) kuwajibika kutekeleza maamuzi ya kisera ya Tume na kazi za kila siku za utawala na uendeshaji wa shughuli za Tume;
(b) kuwajibika kupanga shughuli kwa ajili ya, kutayarisha taarifa na kutunza mihtasari ya maamuzi na mienendo ya mikutano yote ya Tume; na
(c) kufanya kazi nyingine yoyote atakayopangiwa na Tume au kwa au chini ya sheria nyingine yoyote.

(4)Katibu, isipokuwa tu pale ambapo Tume itakapoelekeza vinginevyo kwa maandishi, atahudhuria mikutano yote ya Tume lakini hatapiga kura juu ya jambo lolote linalotakiwa kuamuliwa na Tume katika mkutano wowote.

(5) Kutakuwa na maafisa na watumishi wengine wa Tume wanaoweza kuteuliwa na Tume chini ya kifungu hiki.

(6) Tume, kwa kushauriana na Idara ya Utumishi wa Umma, itawajibika na uteuzi, udhibiti na nidhamu ya maafisa na watumishi wake na inaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma kuachisha kazi.

Sura ya 298

(7) Watumishi wa umma wanaweza, kwa maombi ya Tume, kuazimwa kufanya kazi Tume.

Viapo

**12**.- (1) Kila Kamishna na Katibu Mtendaji wa Tume, kabla ya kuanza majukumu ya kazi yake, atakula kiapo cha utii na kiapo cha kutekeleza majukumu ya

kazi yake kama ilivyoelezwa katika Jedwali la Sheria hii, na watakula viapo hivyo mbele ya Rais.

(2) Mtu yoyote atakayeteuliwa kufanya kazi Tume, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu ya kazi yake, atakula kiapo cha kutunza siri kama ilivyoelezwa katika Jedwali la Sheria hii, na atakula kiapo hicho mbele ya Kamishna.

## SEHEMU YA III

### HADHI, MAMLAKA NA UWEZO WA TUME

Tume idara ya umma Sheria Na. 16 ya 2001 kif.4

**13**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Katiba na Sheria hii, masharti ya sheria yoyote yanayohusu idara za umma yatatumika kwa Tume, na ofisi ya Tume na ofisi yoyote iliyoanzishwa chini ya Tume zitakuwa ni ofisi za umma katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume inaweza, endapo itaona ni muhimu au inastahili, itaanzisha ofisi za matawi nje ya makao yake makuu katika maeneo megine ya kijiografia kama itakavyoona inafaa ni muhimu, na inaweza kuanzisha vitengo au idara na kuzipa majukumu maalum kulingana na majukumu ya Tume;

(3) Kutakuwa na Kamishna Msaidizi au mtu atakayeteuliwa na Tume katika kila ofisi za Tawi kuwa mwakilishi wake.

(4) Kamishna Msaidizi au mwakilishi wa Tume atalazimika-

(a) kupokea malalamiko kutoka kwa umma;

(b) kufanya uchunguzi wa papo hapo kama inavyoweza kuhitajika; na

(c) kutekeleza kazi nyingine zinazohusiana na majukumu ya Tume kama atakavyopangiwa na Tume.

Uhuru wa Tume

**14**.-(1) Isipokuwa kama inavyotamkwa na Katiba, Tume itakuwa ni idara inayojitegemea na Makamishna, katika kutekeleza majukumu yao, hawatakuwa chini ya maelekezo wala udhibiti wa mtu au mamlaka yoyote.

(2) Serikali, mamlaka za umma na vyombo vingine vitatoa usaidizi na ushirikiano kama itakavyohitajika ili kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa masharti ya kifungu kidogo cha (1).

Mamlaka ya Tume

**15**- (1) Tume itakuwa na mamlaka ya kuchunguza uvunjaji wowote wa haki za binadamu au matumizi mabaya ya madaraka-

(a) kwa kuanzisha uchunguzi yenyewe; au

(b) kwa kupokea lalamiko au tuhuma chini ya Sheria hii ya-

(i) muathirika kwa maslahi yake binafsi;

(ii) jumuiya ikiwakilisha maslahi ya wanachama wake; au

(iii) mtu akiwakilisha maslahi ya kikundi au tabaka la watu.

(2) Baada ya kufanya uchunguzi chini ya sheria hii, Tume itakuwa na mamlaka ya-

(a) pale itakapokuwa sahihi, kuhimiza usuluhishi na upatanishi kati ya pande husika; au

(b) kuhakikisha kwamba lalamiko na matokeo ya uchunguzi wa Tume yanawasilishwa kwa mamlaka husika au mtu mwenye udhibiti juu ya mtu ambaye kitendo au mwenendo wake ulichunguzwa na Kamishna; au

(c) kupendekeza kwa mtu stahiki au mamlaka hatua, au kuitaka mamlaka hiyo kuchukua hatua, zitakazotoa suluhisho linalofaa, nafuu au marekebisho.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha 2 cha kifungu hiki, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake chini ya Katiba na Sheria hii, Tume inaweza kufungua shauri mahakama yoyote na inaweza kuomba nafuu ambayo inaweza kutolewa na mahakama hiyo.

Ukomo na Mipaka ya uchunguzi

**16.**-(1) Masharti ya Ibara ya 46 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 36 ya Katiba ya Zanzibar vinaizuia Tume, na Tume haitakuwa na mamlaka ya kuchunguza au kuanzisha mashtaka yoyote dhidi ya Rais au Rais wa Zanzibar.

(2) Tume haitachunguza-

(a) jambo ambalo liko mahakamani au chombo kingine chenye asili ya mahakama;

(b) jambo linalohusu uhusiano au mashirikiano kati ya Serikali na Serikali ya nchi yoyote ya kigeni au taasisi ya kimataifa;

(c) jambo linalohusu mamlaka ya Rais ya kutoa msamaha;

(d) jambo ambalo Rais ataelekeza vinginevyo kwa mujibu masharti ya Katiba.

(3) Endapo Rais ameamua kuielekeza Tume kutofanya uchunguzi kwa masharti ya Katiba na Sheria hii, ataelekeza hivyo kwa maandishi na

kutoa sababu kwa Tume kuhusu zuio hilo na Tume itamjulisha mlalamikaji ndani ya siku 30 za maamuzi, ikiwa yupo, kuhusu uamuzi huo na sababu zake.

(4) Maagizo yoyote kama hayo yatafanywa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 130 ya Katiba ikiwa Rais ataona kwamba kuna hatari halisi na kubwa kwamba uchunguzi ungeathiri masuala ya ulinzi, au usalama wa taifa.

(5) Hakuna masharti katika kifungu hiki yanayomaanisha kumzuia mtu yeyote kutafuta nafuu vinginevyo katika Mahakama Kuu chini ya masharti ya Ibara ya 30(3) ya Katiba.

Hadhi ya mienendo, maamuzi na mashahidi

**17.-(1)** Maamuzi ya Tume yatakuwa na hadhi ya mapendekezo kwa mamlaka husika au mtu mwenye udhibiti wa mtu ambaye matendo au mwenendo wake umechunguzwa.

(2) Mienendo ya mashauri ya Tume na maamuzi yake na taarifa yoyote, nyaraka au kitu kilichowasilishwa na mtu yoyote kuhusiana na uchunguzi chini ya Sheria hii kitapewa hadhi sawa na mienendo na masuala mengine mbele ya mahakamani.

(3) Hakuna uchunguzi, mwenendo au mchakato wa Tume utakaokuwa batili kwa sababu tu ya dosari au kutozingatia utaratibu, isipokuwa kwa sababu ya kutokuwa na mamlaka, hakuna uchunguzi, mwenendo, mchakato au taarifa ya Tume itakayoweza kupingwa, kufanyiwa mapitio, kutupiliwa mbali au kuhojiwa katika mahakamani yoyote.

(4) Hakuna mashtaka yatakayofunguliwa dhidi ya Makamishna, maafisa na watumishi wa Tume na watu wengine waliopewa mamlaka na Tume kuhusiana jambo lolote walilofanya au kutofanya wakati wa kutekeleza majukumu yao chini ya Sheria hii isipokuwa kama itaoneshwa kwamba jambo hilo limefanywa au halikufanywa kwa nia ovu.

(5) Hakuna Kamishna au mtu yeyote aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (4) atakayeitwa kutoa ushahidi katika mahakama yoyote au katika mashtaka mengine yoyote yenye asili ya kimahakama kuhusiana na mienendo katika uchunguzi wowote au jambo lolote analolifahamu wakati anatekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii.

(6) Hakuna masharti katika Kifungu kidogo cha (4) au (5) yatakayotumika katika mashtaka kwa kosa chini ya Sheria ya Usalama wa Taifa, kwa kosa kinyume na vifungu vya 102, 103, 106, 108, au 109 vya Kanuni ya Adhabu kuhusiana na uchunguzi, au kwa kosa kinyume na kifungu cha 37

cha Sheria hii.

(7) Shahidi mbele ya Tume atakuwa na haki sawa na shahidi mbele ya Mahakama Kuu

Usikilizaji mashauri hadharani

**18.** Kwa kuzingatia kifungu cha 19, mwenendo wakati wa uchunguzi mbele ya Tume utafanywa hadharani.

Uficho na Usiri
Sheria Na. 16 ya 2001 kif. 5

**19.-**(1)Tume inaweza, kwa uamuzi wake yenyewe au kwa kuombwa, kuchukua hatua zinazofaa na kutoa amri yoyote itakayoona ni muhimu kuhakikisha usiri wa uchunguzi au sehemu yoyote ya uchunguzi ikiwa, baada ya kuzingatia hatua zote mbadala zilizopo, Tume imejiridhika kwamba-

(a) kuna hatari halisi na kubwa ambayo-

(i) ufichuzi ungeathiri usalama wa taifa au uhuru wa Nchi, ulinzi wake au uhusiano wa kimataifa;

(ii) chanzo cha siri cha taarifa kuhusiana na uchunguzi au katika utekelezaji wa sheria ya jinai kingetambuliwa au kuhatarishwa; au

(iii) haja ya kufanya uchunguzi au sehemu ya uchunguzi hadharani inazidi maslahi ya kuficha siri;

(b) kuna uwezekano kwamba maisha, uhuru au usalama binafsi wa mtu au maslahi ya watu wanaoweza kupata madhara, wakiwemo watoto yatahatarishwa.

(2) Tume inaweza kukataza au kuzuia kuchapisha ushahidi wowote uliotolewa mbele yake au utambulisho wa mtu yeyote ikiwa itaona kwamba sababu za kutoa amri ya katazo au zuio zinauzito zaidi ya maslahi ya umma katika kuchapisha ushahidi au utambuliso huo.

(3) Kila mjumbe wa Tume na kila mtu aliyeajiriwa na Tume atalazimika kuchukua tahadhari zinazofaa kuepuka kuweka wazi jambo lolote ambalo kuwekwa kwake wazi kumekatazwa au kuzuiwa na Tume chini ya kifungu kidogo cha (1) au kifungu kidogo cha (2).

Utaratibu wa kusikiliza shauri

**20.-**(1) Tume itakuwa na mamlaka ya kuamua yenyewe utaratibu wake wa kusikiliza masuala yaliyowasilishwa mbele yake lakini inaweza vinginevyo kuongozwa na taratibu hizo kama zinavyoweza kuwa zimefafanuliwa na kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Katika kufanya uchunguzi, Tume itazingatia misingi ya haki ya asili lakini haitalazimika kufungwa na taratibu zozote za kisheria na kiufundi za ushahidi zinazotumika katika mashtaka yaliyo mbele ya mahakama; na mienenendo yote ya mashauri itafanyika kwa taratibu zisizo rasmi na kwa

haraka.

(3) Katika mienendo ya mashauri chini ya Sheria hii, uamuzi wa wajumbe wengi waliohudhuria kikao, ikiwa wajumbe waliohudhuria wanatimiza akidi, utakuwa ni uamuzi wa Tume; na endapo kutakuwa na mgongano wa kura katika suala lolote, mjumbe anayeongoza kikao atakuwa na kura ya uamuzi mbali ya kura yake ya kawaida.

Vikao na Maamuzi ya Tume
Sheria Na. 16 ya 2001 kif. 6

**21.-**(1) Vikao vya Tume vitaongozwa na Mwenyekiti au kama Mwenyekiti hayupo vitaongozwa na Makamu Mwenyekiti na kama wote hawapo, Makamishna waliopo watamteua mmoja wao kuongoza kikao.

(2) Akidi kwa ajili ya kikao cha Tume itafikiwa kwa kuwepo zaidi ya nusu ya wajumbe wa Tume mbali na Makamishna Wasaidizi, na pale ambapo kikao hakitafanyika kwa kukosa akidi inayotakiwa ya Makamishna, Kamishna Msaidizi anaweza kualikwa kuhudhuria kwa lengo la kukidhi akidi.

(3) Kikao cha Tume kwa lengo la kufanya uchunguzi, kitaundwa na Kamishna mmoja na maafisa waandamizi wa Tume wasiopungua wawili kama wanavyoweza kuteuliwa na Tume kwa kigezo cha uelewa wao, uzoefu na ustadi wa kushughulikia jambo linalochonguzwa.

(4) Kikao cha Tume kwa lengo la kufanya uchunguzi kitakuwa na uhalali kama kitamhusisha Kamishna Msaidizi na maafisa waandamizi wawili.

## SEHEMU YA IV

## MALALAMIKO NA CHUNGUZI

Namna ya kuwasilisha malalamiko
Sheria Na. 16 ya 2001 kif. 7

**22.**–(1) Malalamiko yote yanaweza kuwasilishwa Tume kwa mdomo au kwa maandishi na yatasajiliwa kwa namna itakayoelekezwa na Tume.

(2) Kwa kuzingatia sheria yoyote husika endapo barua imeandikwa na-
(a) mtu ambaye yuko kizuizini; au
(b) mgonjwa aliyepo hospitali,
imeelekezwa kwa Tume, itawasilishwa Tume mara moja bila kubadili chochote na mtu aliyeaminiwa.

(3) Lalamiko chini ya Sheria hii linaweza kuwasilishwa na mtu binafsi au kikundi cha watu kilichosajiliwa au kisichosajiliwa.

(4) Tume itashughulikia kila lalamiko lilowasilishwa mbele yake isipokuwa pale Tume itakavyojiridhisha kuwa-
(a) lalamiko linahusu uamuzi, pendekezo, tendo au upungufu ambao mlalamikaji alikuwa anafahamu kwa zaidi ya miezi 24 kabla ya lalamiko kupokelewa Tume; au
(b) Mdaiwa wa uathirika wa kitendo au matendo yanayolalamikiwa alipaswa kufuata mikondo au taratibu nyingine zilizoelekezwa na

sheria zilizopo;
(c) lalamiko ni la kipuuzi , kuudhi au limefanywa kwa nia ovu; au
(d) lalamiko linaangukia nje ya mamlaka ya Tume.

(5) Tume inaweza kushughulikia lalamiko lolote ambalo ingeweza kulikataa kwa sababu kuwa mlalamikiwa alikuwa analifahamu zaidi ya miezi 24 kabla ya kupokelewa Tume kama –
(a) Kwa lengo la kuhakikisha kuwa mwisho wa haki unapatikana, vinginevyo itakuwa bora kushugulikia lalamiko badala ya kulikataa; au
(b) lalamiko lina umuhimu wa kikatiba; au
(c) kwa kuzingatia kiini cha lalamiko na mazingira yanayomzunguka mlalamikaji,

Tume imejiridhisha kuwa italishughulikia lalamiko hilo.

Uwakilishi

**23**.-(1) Mlalamikaji, upande wenye maslahi na mtu mwingine yoyote ambaye mwenendo au tendo lake kuna uwezekano wa kuathiriwa na maoni ya Tume anaweza kuwakilishwa na wakili au mtu mwingine yeyote anayefaa kumwakilisha Tume.

(2) Endapo mtu ambaye lalamiko lake lingeweza kufanywa chini ya Sheria hii amefariki au ni, kwa sababu yoyote ya kutosha, hawezi kujishughulikia yeye binafsi, lalamiko linaweza kufanywa na mwakilishi wake binafsi au na mwanafamilia yake au mtu mwingine anayefaa kumwakilisha.

Taarifa ya lalamiko na fursa ya kusikilizwa

**24.** Baada ya lalamiko kupokelewa na Tume, Tume itamtaarifu mlalamikiwa na, upande mwingine wowote na itazipa fursa za kutosha pande zote zenye maslahi zilizopewa taarifa ya wito, kwa mtu binafsi au kupitia mwakilishi, kwenye uchunguzi na kutoa ushahidi na kufanya uwakilishi.

Mamlaka Maalum ya uchunguzi

**25**. Tume kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, itakuwa na mamlaka-
(a) kutoa wito au amri nyingine kumtaka mtu yeyote kuhudhuria mbele yake na kuwasilisha nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote katika upelelezi au uchunguzi ambacho kinaweza kuwa katika umiliki au udhibiti wa mtu huyo;
(b) kumhoji, kwa kiapo au uthibitisho, mtu yeyote kuhusiana na jambo lolote linalochunguzwa;
(c) kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa yoyote anayofahamu kuhusiana na upelelezi au uchunguzi;
(d) kutoa amri za muda ili kulinda, ikisubiriwa uamuzi wa mambo yanayobishaniwa kwa wakati huo kati ya pande zinazobishana kwenye mienendo au haki za pande husika;
(e) kwa kuzingatia sheria nyingine yoyote, kuingia na kufanya upekuzi,

katika maeneo yoyote muhimu kwa uchunguzi na kuchukua nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote kinachofaa; na

(f) kumfanya, mtu yoyote anayedharau mienendo ya mashauri au amri zake kufunguliwa mashataka kwenye mahakama yenye uwezo kisheria.

Utaratibu wa kufanya Uchunguzi

**26.-**(1) Pale ambapo Tume inaamua kufanya uchunguzi chini ya Sheria hii, itaipa mamlaka au mtu anayehusika na kwa mtu mwingine yeyote anayetuhumiwa katika lalamiko kuchukua au kuridhia kitendo kinacholalamikiwa kutofanyika, fursa ya kutoa maoni juu ya tuhuma zozote zilizomo kwenye lalamiko na mwakilishi wa mamlaka au mtu anayehusika atawasilisha maoni yake ndani ya muda ambao Tume inaweza kuutaja.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu hiki, Tume inaweza kupata taarifa kutoka kwa watu hao na kwa namna ambayo, na kufanya udadisi kama itakavyoona ni lazima.

Ushahidi wakati wa uchunguzi.

**27.-**(1) Kwa kuzingatia kifungu hiki, Tume inaweza kumtaka mtu yeyote ambaye, kwa maoni yake, anaweza kutoa taarifa yoyote kuhusiana na jambo linalochunguzwa na Tume –

(a) kuipatia taarifa;

(b) kutoa nyaraka yoyote, andiko au kitu ambacho kwa maoni yake kinahusiana na jambo ambalo linachunguzwa na ambacho kinaweza kuwa kwenye umiliki au udhibiti wa mtu huyo.

(2) Tume inaweza kumuita kwa wito mbele yake na kumhoji kwa kiapo au tamko–

(a) mtu anayetakiwa kutoa taarifa au kuwasilisha kitu chochote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki;

(b) mlalamikaji;

(c) mtu mwingine yoyote ambaye Tume inaona ataweza kutoa taarifa inayohitajika chini ya kifungi kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mtu yeyote aliyeitwa na kufika mbele ya Tume kama shahidi anastahili kulipwa kwa njia ya kurejeshewa gharama zake, posho kama zinazolipwa kwa shahidi anayefika mbele ya Mahakama Kuu katika mashauri ya jinai.

(4) Mtu yeyote aliyealikwa na Tume kuhudhuria kikao chochote cha Tume anaweza kulipwa posho kwa namna Tume itakavyoona inafaa.

Utaratibu baada ya uchunguzi.

**28.-**(1) Pale ambapo baada ya kufanya uchunguzi chini ya Sheria hii, Tume ina maoni kwamba uamuzi, pendekezo, kitendo kilichofanywa au kutofanywa kuhusu jambo lililokuwa linachunguzwa–

(a) linasababisha uvunjifu wa haki zozote za msingi na uhuru unaotamkwa kwenye Katiba au kwenye mkataba wowote wa kimataifa ambao Jamhuri ya Mungano imeridhia.

(b) linaonekana lilikuwa kinyume cha sheria; au

(c) halikuwa na maana, siyo la haki, kandamizi, la kibaguzi au lilikuwa ni kwa mujibu wa utawala wa sheria au sharti la yoyote , au mazoea yasiyofa, yasiyo ya haki, kandamizi, au ya kibaguzi; au

(d) lilizingatia kabisa au kwa sehemu makosa ya kisheria au ukweli wa jambo; au

(e) lilizingatia kwenye sababu zisizohusika au kufanywa kwa lengo lisilofaa; au

(f) lilifanywa katika utekelezaji wa kiutashi na sababu za maamuzi zilipaswa kutolewa Tume itatoa taarifa ya uamuzi wake, pendekezo na sababu za kufanya hivyo kwa mamlaka inayohusika.

(2) Mamlaka husika itatakiwa, ndani ya muda usiozidi miezi mitatu tangu tarehe ya pendekezo kwa namna Tume itavyofafanua, kutoa taarifa kwa Tume yenye maelezo ya kina ya hatua yoyote iliyochukuliwa na mamlaka hiyo kurekebisha haki za msingi zilizoingiliwa au vitendo vya matumizi mabaya ya madaraka.

(3) Ikiwa ndani ya kipindi kilichofafanuliwa baada ya taarifa kutolewa hakuna hatua iliyochukuliwa ambayo itaonekana kwa Tume kutosheleza na kustahiki, Tume, inaweza baada ya kuzingatia maoni, kama yapo, yaliyofanywa na au kwa niaba ya idara, mamlaka au mtu aliyekuwa analalamikiwa aidha, kufungua shauri mahakama yoyote au kupendekeza kwa mamlaka yoyote yenye uwezo wa kufungua shauri na kuomba nafuu kama hizo kwa namna itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa mapendekezo ya Tume.

(4) Masharti ya kifungu hiki hayatatafsiriwa kuwa yanaizuia Tume kutatua lalamiko lolote au kurekebisha kitendo chochote au upungufu unaotokana na ukiukwaji wa haki yoyote ya kimsingi au vitendo vya matumizi mabaya madaraka kwa namna nyingine ikiwemo usuluhishi, upatanishi na majadiliano.

## SEHEMU YA V

### FEDHA, UKAGUZI NA TAARIFA

Rasilimali za Tume

**29.** Mapato ya Tume yatahusisha fedha-

(a) zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Tume;

(b) zilizoongezwa Tume kutoka chanzo kingine chochote; au

(c) ambazo ni michango au misaada kutoka vyanzo vya ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano.

Uwajibikaji

**30**.-(1) Tume itawajibika kwa Bunge katika hesabu kwa mapato na matumizi yake yote.

(2) Tume itatakiwa –

(a) kutunza kumbukumbu kamilifu na sahihi za mapato na matumizi yake yote na za mali zote, madeni na shughuli zote za kifedha;

(b) kujiridhisha yenyewe kwamba hatua zote sahihi za usimamizi zimechukuliwa kuhakikisha kwamba rasilimali ambazo ni muhimu kwa kufanikisha malengo yake kwa jinsi inavyowezekana, zinapatikana, zinalindwa na kutumika kwa uangalifu, ufanisi na namna inayofaa;

(c) kuandaa hesabu za matumizi kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma; na

(d) kuandaa hesabu za mwaka kwa kuzingatia taratibu za kiuhasibu kwa ujumla zilizokubalika, zinazohusisha shughuli zake zote.

Makadirio ya mapato na matumizi

**31. –** (1) Tume, kwa kuzingatia mwaka wake wa kwanza wa fedha chini ya Sheria hii na kwa kila mwaka wa fedha utakaofuata, itaandaa na kuwasilisha kwa Waziri makadirio ya mapato na matumizi yake na Waziri atapitia makadirio hayo na kuyawasilisha Bungeni.

(2) Katika uandaaji wa makadirio yake chini ya kifungu kidogo (1), Tume itazingatia ushauri wa Waziri na Waziri anayehusika na masuala ya Fedha.

Ukaguzi wa hesabu

**32.-** (1) Hesabu za Tume zitakaguliwa, mara moja kila mwaka wa fedha, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

(2) Baada ya kumaliza ukaguzi wake wa hesabu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atathibitisha hesabu hizo na kuwasilisha taarifa yake Tume.

Taarifa za mwaka
Sheria Na. 19 ya 2004

**33.-** (1) Tume, ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, itaandaa na kuwasilisha kwa Bunge kupitia kwa Waziri anayehusika taarifa ya mwaka kwa mwaka huo iliyojumuisha-

(a) nakala ya hesabu za Tume zilizokaguliwa pamoja na taarifa ya mkaguzi kuhusu hesabu hizo;

(b) taarifa kuhusu shughuli za Tume katika mwaka huo wa fedha; na

(c) taarifa nyingine ambazo Waziri anaweza kuhitaji,

na Waziri ataipeleka taarifa, kwa ajili ya kujadiliwa, mbele ya Bunge.

(2) Tume pia itawasilisha nakala ya taarifa ya mwaka kwa Rais na Rais wa Zanzibar.

Taarifa maalum

**34.** Tume wakati wowote inaweza, ikiwa inaonekana inafaa kwa Tume, kuwasilisha taarifa maalum kwa Waziri, kuhusu jambo lolote linaloambatana na utendaji wa majukumu yake.

Taarifa nyingine

**35.** Tume inaweza, kwa maslahi ya umma au kwa maslahi ya mtu yeyote au mamlaka kuandaa na kuwasilisha taarifa zinazohusiana na-

(a) kwa ujumla utekelezaji wa majukumu yake;

(b) jambo lolote ambalo linahitaji Rais, Rais wa Zanzibar, Waziri, Bunge au mtu mwingine yeyote au mamlaka ijulishwe; au

(c) shauri lolote mahsusi lililochunguzwa na Tume, ikiwa au la ni masuala yaliyomo katika taarifa iliyowasilishwa Bungeni.

## SEHEMU YA VI

## VIFUNGU ANUAI

Utaratibu n.k. wa Tume

**36.** Kwa kuzingatia Sheria hii na kanuni yoyote iliyotungwa chini yake, Tume inaweza kuratibu matendo yake, utaratibu na masuala yanayohusiana na vikao na uchunguzi.

Makosa na adhabu

**37.** (1) Mtu anatenda kosa la jinai na anawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja kama mtu huyo, kuhusiana na utekelezaji wa jukumu lolote la Tume chini ya Sheria hii-

(a) anadhoofisha, anaingilia, kunyanyasa, kuingilia kati au kufanya ushawishi usiofaa kwa, mjumbe wa Tume, mtumishi wa Tume au mtu anayeteleza majukumu yoyote ya Tume;

(b) bila sababu za kisheria au za msingi, anakataa au anashindwa kufika mbele ya Tume baada ya kuitwa kwa wito au kula kiapo au kutoa tamko kwa ombi la Tume, au kukataa kujibu maswali yoyote baada ya kuamriwa kufika mbele ya Tume;

(c) anatoa taarifa ya uwongo au ya kupotosha au ushahidi kwa Tume kuhusu jambo lolote, akijua kuwa taarifa au ushahidi huo kuwa ni wa uwongo au kutoujua au kuuamini kwamba ni wa ukweli; au

(d) anamtishia au kumwathiri mtu anayetoa taarifa, ushahidi au msaada kwa Tume;

(e) bila sababu za kisheria au mamlaka anakataa au kupuuza kutekeleza pendekezo lolote lililotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu cha 28 cha Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1)(e) endapo kosa la jinai limetendwa na-

(a) shirika, kila mkurugenzi, mtendaji mkuu au afisa mwingine wa chombo ambaye anawajibika na utekelezaji wa pendekezo atakuwa na hatia ya kutenda kosa hilo;

(b) ubia, kila mbia anayehusika na utekelezaji wa pendekezo atakuwa na hatia ya kutenda kosa hilo; na

(c) mamlaka ya umma, afisa au maafisa waliopewa jukumu la kutekeleza pendekezo na kutoa taarifa kuhusu pendekezo hilo watakuwa na hatia ya kosa hilo.

Kanuni

**38.** Waziri anaweza kutunga kanuni za utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufutwa kwa Sheria Na. 25 ya mwaka 1966

**39.** Sheria ya Tume ya Kudumu ya Uchunguzi, 1966 imefutwa.

Muda wa mpito

**40.** Bila kujali kufutwa kwa Sheria ya Tume ya Kudumu ya Uchunguzi ya mwaka 1966, lalamiko lolote au uchunguzi unaoendelea mbele ya Tume hiyo mara kabla ya kuanza kwa Sheria hii utaendelezwa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JEDWALI

***Chini ya Kifungu cha 12(1) na (2)***

### KIAPO CHA WAJUMBE

Mimi ……………………………………, naapa/nathibitisha kwamba. nitatekeleza.majukumu ya Mjumbe wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa uhuru bila woga, upendeleo, huba au hila, na kwamba, sitatoa siri zozote nitakazozifahamu wakati nikitekeleza majukumu yangu bila kibali cha Tume isipokuwa katika kutekeleza majukumu ya Tume,

MUNGU NISAIDIE

Kiapo/tamko limetolewa mbele yangu leo tarehe……………………mwezi……………….2001

………………………………..
*Rais*

### KIAPO CHA WATUMISHI WA TUME

Mimi………………………………………., naapa/ nathibitisha kwamba sitatoa siri zozote moja kwa moja au kwa namna nyingine kwa mtu yeyote ambaye haruhusiwi isipokuwa katika utekelezaji wa majukumu yangu nyaraka, mawasiliano au taarifa zozozte nitakazozifahamu

wakati nikitekeleza majukumu yangu kama mtumishi wa Tume au kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Sura 931

MUNGU NISAIDIE

Kiapo/Tamko limetolewa mbele yangu leo tarehe……………mwezi…………………….20……………..

……………………………..
*Kamishna*

Imepitishwa Bungeni tarehe 28 Machi, 2001

**KIPENKA M. MUSSA,**
*Katibu wa Bunge*